HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MPANGO WA USIMAMIZI WA MISITU

KIJIJI CHA MTAWATAWA

MUHUTASARI

Utangulizi

Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 inatoa kipaumbele kwa jamii kushirikishwa katika usimamizi wa misitu. Pia sera inasisitiza mchango wa sekta ya misitu katika kukuza kipato cha jamii ili kupunguza umasikini. Ufupisho huu unaelezea vipengele muhimu vya usimamizi wa msitu wa kijiji Mtawatawa utakaotumika katika kipindi cha miaka mitano. Lengo la nikuwezesha kutoa uelewa wa haraka uliopo ndani ya mpango

Umiliki wa msitu

Msitu unamilikiwa na Serikali ya kijiji cha Mtawatawa na ulitengwa kuwa hifadhi tarehe 06 Mei 2005 chini ya usaidizi wa kitalaamu kutoka kwa wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale na Idara ya misitu na Nyuki wakishirikiana na serikali ya Finland kupitia mradi wa RIPS (Rural Integrated Project Support).

Lengo kuu la mpango wa usimamizi

Msitu wa kijiji ulitengwa kwa lengo kuu la kuhifadhi msitu katika hali ya uhalisia na kuboresha hali ya maisha ya kizazi kilichopo na kijacho kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za Misitu.

Madhumuni

- Kuhifadhi eneo la msitu lenye ukubwa wa hekta 12,391 dhidi ya ukataji miti ovyo, uharibifu na matumizi yasiyofaa.
- Kuhakikisha kuwepo na upatikanaji wa mazao yasiyotimbao kwa wakati wote kwa ajili ya matumizi ya kawaida.
- Kuhifadhi uoto wa asili wa msitu na bionuai kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.
- Kuwezesha kijiji cha Mtawatawa kupata mapato kutokana na uvunaji endelevu wa rasilimali za misitu.
- Kuboresha hali ya maisha ya wanajamii wa kijiji cha Mtawatawa .

Maelezo kuhusu msitu

Jina la msitu

Msitu wa hifadhi wa kijiji cha Mtawatawa unaitwa Mbila.

Mahali ulipo Msitu na ukubwa wake

Msitu wa hifadhi wa **Mbila** una ukubwa wa hekta 12,391 na upo upande wa Kusini katika ardhi ya kijiji. Unapakana na vitongoji vya Mageuzi, Raha leo, Nanyumbu, Kipule na Mkongoteka. (Angalia Kiambatisho A(i) ramani inayoonyesha mipaka ya msitu wa kijiji) Msitu unafikika kwa kupitia njia ya Nasibu na barabara ya mkwajuni.

Matumizi ya maeneo yanayozunguka msitu ni kama ifuatavyo

- Upande wa Kaskazini ni eneo la kilimo na malisho.
- Upande wa Kusini kuna msitu wa hifadhi wa kjiji cha Nahoro
- Upande wa Mashariki kuna msitu wa hifadhi wa kjiji cha Kitogoro.

- Upande wa Magharibi ni msitu wa hifadhi wa kijiji cha Legezamwendo.

Jamii za miti ya mbao

Kuna aina nyingi za jamii tofauti za miti. Jamii za miti ya thamani ya mbao zilizopo msituni ni:- Mninga jangwa (*Pterocarpus angolensis*), Mkongo (*Afzelia quanzesis*), Mpingo (*Dalbegia melanoxylon),* Msekeseke (*Bobgunnia madagascariensis*)), Mtondoro (*Julbenadia globiflora*), Mninga bonde (*Pterocarpus holtzii*), Mlipadeni , Msufi pori (*Bombax rhodognaphalon*), Mkarati (*Burkea africana),* Myombo (*Branchystegia longifolia)* Mchenga (*Branchystegia spiciformis*), Mpangapanga *(Millettia stuhlmannii).* Mneke, Mkunya, Mtumbu, Kimbilia,, Mwengere, Mmanga, Mmalala, Mlondondo , Mndwenje, Mkalakawa, Mpembarati, Mnidu, Mpuga, Mtanga, Mkulakula, Migeregere, Kingonogo, Mhani na Mmelendende.

Mazao yasiyotimbao

Kuna aina mbalimbali za mazaoyasiyotimbao kama vile uyoga, viazi pori (angadi, mong'oko, upupu pori), madawa ya asili, kamba, miyaa, na nyasi.

- Miti inayofaa kwa ujenzi ni Mchenga, Mneke, Mnyadi, Mpalangwale, Mpugupugu, Mtandawala, Mianzi, Mkwaju, Kimbilia, Kingonogo na Mnyandu.
- Miti ya matunda ni Mdawa, Mbingi, Mahilu, Matopetope, Usufo, Mfulu, Vitoro, Mhanga, Undaunda, Mpalangwale, Mang'ombe na Mbulukututu..
- Miti inayotumika kutengenezea kamba ni Mchenga, Mpugupugu, Miyombo, Ngwalengwale, Makungu, Mneke, Mwengere na Mtumbu.
- Jamii za uyoga zifuatazo zinapatikana katika msitu huu Lingujugu, Minjecheche, Lipoa, Uyoga ubuyu, Ungangalakata, Ulelema, Uwinda, Utumbati, Ugongolo, Lipikamambwe, Utembo, Uchinji na Mngolobele

Wanyama pori na jamii za ndege

Pundamilia, Mbawe, Mbalapi, Nungununungu, Nenje, Mbunju, Kakakuona, Kiboko, Kobe, Mikuli, Kikululu, Ndonda, Kikui, Mbendu, Bweha, Kenge, Chatu, Njudi, KombaSungura, Tandala, Paa, Nyati, Simba, Chui, Tembo, Nyani, Tumbili, Fisi, Kima, Mbwa mwitu, Ngolombwe, Mbawala, Towe, Nguruwe na Ngiri .

Maeneo ya Usimamizi

Msitu huu umegawanyika katika maeneo madogo ya usimamizi

Eneo la kwanza ni eneo la uhifadhi lina ukubwa wa hekta **1,239** ambazo ni sawa na asilimia 10(%) ya msitu mzima na limetengwa kama eneo ambalo uvunaji wa miti hauruhusiwi kabisa kufanyika.

Eneo la pili ni eneo la uvunaji lenye ukubwa wa hekta **11,152** ambazo ni sawa na asilimia 90 (%) ya msitu mzima. Eneo hili limefanyiwa tathmini ya rasilimali za Msitu na Mpango wa uvunaji endelevu umeandaliwa na hakuna uvunaji wa miti utakaofanyika bila kufuata mpango huo.

Matumizi ya msingi

Wanajamii wa kijiji cha Mtawatawawatakuwa na haki ya kuingia katika msitu wa jamii bila kibali kupata matumizi ya msingi ya kufanya matambiko, maji na kupita njia

zinazofahamika, haki hii itahusu vijiji jirani piaWasio wakazi wa kijiji hawataruhusiwa katika maeneo ya kijadi bila uangalizi wa kamati ya Maliasili.

Matumizi huru ya msitu

Matumizi huru kwa wanakijiji wa Mtawatawayatakuwa kwa ajili ya mazao yasiyotimbao,kama asali ya nyuki wasiouma, uyoga, kuni, majengo, matundapori, madawa ya asili na kutundika mizinga, vyote hivyo vitapatiwa kibali maalum cha bure kutoka serikali ya kijiji.

Wasio wakazi wa kijiji cha Mtawatawawanaweza pia kuomba kibali toka serikali ya kijiji kutumia mazao yaliyotajwa hapo juu toka msitu wa kijiji. Kamati ya maliasili itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mazao ya msitu yanayotolewa bure yanatumiwa kiendelevu na hayamalizwi toka msitu wa jamii. Watumiaji wa nje ya kijiji wanaotaka kuvuna mazao haya kwa ajili ya biashara wanaweza kutozwa ushuru kama ilivyopangwa na Kamati ya Maliasili.

Shughuli zifuatazo zitatozwa ushuru na serikali ya kijiji.

- Kutembelea msitu kwa ajili ya mafunzo.
- Utafiti.
- Utalii msituni.

Mazao Yanayohitaji Vibali vya Uvunaji

Kabla ya kuvuna jamii yeyote ya miti iliyoorodheshwa, lazima tathmini ifanyike ili kubaini kiasi kilichopo na mpango wa uvunaji utatayarishwa. Tathmini ya kina itafanyika kufuatana na mwongozo wa Tathmini Shirikishi ya rasilimali za misiti wa Idara ya Misitu na Nyuki katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Taarifa za Tathmini shirikishi zimeambatanishwa katika mpango huu. Tathmini shirikishi haitafanyika katika eneo lililotengwa Kwa ajili ya hifadhi (eneo la 10% la msitu).

Mpango wa uvunaji utaelezea namna kiwango cha uvunaji kilivyopatikana kutokana na matokeo ya tathmini na utabainisha ni kwa namna gani kiwango hicho ni endelevu. Mpango wa uvunaji ni lazima upitishwe na kamati ya maliasili na kuambatanishwa katika mpango huu.

Mazao mengine ya misitu

Mazao mengine yote yatalipiwa ushuru sawa na sheria ndogo ya kijiji husika ila ada hiyo isizidi viwango vya sheria mama.

Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya msitu

- Uvunaji wa miti ya mbao ambayo haijatengenezewa mpango wa uvunaji.
- Kilimo ndani ya msitu
- Makazi ndani ya msitu
- Kuchoma moto ovyo
- Kuchoma moto bila kibali

Shughuli za Kuendeleza na Kutunza Msitu

Mikakati ya jumla ya kutunza na kuendeleza misitu pamoja na rasilimali zake imewekwa bayana. Mambo yatakayoangaliwa ni utunzaji wa misitu hii ili isiharibiwe dhidi ya kilimo na moto. Ulinzi wa msitu, kinga na uthibiti wa moto pamoja na mpango wa matumizi endelevu wa mazao ya msitu utazingatiwa.

Usimamizi wa msitu wa kijiji utakuwa chini ya serikali ya kijiji na utatunzwa na wanajamii wote. Msitu utalindwa na jamii kuzingatia mipaka yake, kila mtu atatoa taarifa kwa uongozi wa kijiji au kamati ya maliasili au kikosi cha doria pale anapoona uharibifu katika msitu. Kamati ya maliasili itaratibu na kusimamia shughuli za doria.

Kutakuwa na timu ya doria itakayochaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji ambayo itakuwa na jukumu la kufanya doria za mara kwa mara katika msitu wa jamii.

Vyanzo vya mapato

- Kutakuwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo toka msitu wa jamii:
- Ada za vikundi vilivyoko mafunzoni,
- shughuli za utafiti na utalii
- Faini za wahalifu
- Ushuru
- Ada za leseni naMengineyo
- Mgawanyo wa Mapato kwa wadau.

Mgawanyo wa mapato yatokanayo na msitu

Mgawanyo wa mapato yatokanayo na mazao ya msitu utakuwa kati ya kamati ya maliasili ya kijiji, Serikali ya kijiji na Halmashauri ya Wilaya. Mgawanyo huu utazingatia nani mwenye majukumu makubwa zaidi katika kutunza na kuendeleza msitu.Katika mkutano mkuu wa kijiji wananchi walikubaliana kuwa asilimia hamsini (50%) ya mapato yaende kwenye serikali ya kijiji kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya kijiji, asilimia arobaini (40%) ya mapato yaende kwa kamati ya Maliasili kwa ajili ya kusimamia na kuendesha msitu na asilimia kumi (10%) ya mapato yaende kwa Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya kutoa ushauri wa kitaalamu pamoja na ufuatiliaji.

Matumizi ya mapato

Mapato yatokanayo na msitu yataelekezwa katika shughuli za;

- Kuendeleza shughuli za msitu zilizopangwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Mapato yatakayobaki yatapelekwa kwa serikali ya kijiji ili yatumike katika shughuli za maendeleo ya jamii.

Matumizi halali ya mapato yatokanayo na msitu wa jamii ni:

- Kulipa motisha (posho) kwa doria.
- Vifaa muhimu kwa ajili ya kuendeleza shughuli za msitu kama ilivyobainishwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Matumizi mengine ya ziada ya kuendeleza msitu yaliyoidhinishwa na Serikali ya kijiji.
- Ununuzi wa vitabu kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za shughuli za msitu.
- Kuchangia katika shughuli za maendeleo kijijini.
- Asilimia arobaini **(40%)** ya mapato yatakuwa kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa msitu chini ya kamati ya Maliasili ya kijiji kwa kiasi kinachokidhi gharama za uendeshaji wa kamati.

Asilimia hamsini**(50%)** iliyobaki itabaki kwa halmashauri ya kijiji kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo ya jamii.

Matumizi halali ya mapato yatokanayo na msitu wa jamii ni:

- Kulipa motisha (posho) kwa doria.
- Kununuavifaa muhimu kwa ajili ya kuendeleza shughuli za msitu kama ilivyobainishwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Matumizi mengine ya ziada ya kuendeleza msitu yaliyoidhinishwa na Serikali ya Kijiji.
- Ununuzi wa vitabu kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za shughuli za msitu.
- Kuchangia katika shughuli za maendeleo kijijini.

Usimamizi wa Fedha

Fedha zote zitatunzwa benki isipokuwa kwa fedha chache kwa ajili ya matumizi madogomadogo. Fedha ndogondogo hazitakiwi kuzidi shilingi 100,000/= Kutakuwa na akaunti benki itakayofunguliwa kwa jina la **Akauti ya Maliasili ya Kijiji cha Mtawatawa**na itakuwa na watia sahihi

Taarifa ya Mapato na Matumizi

Kamati ya Maliasili itatoa taarifa ya Mapato na Matumizi kila mwezi kwa Serikali ya Kijiji na kila baada ya miezi mitatu kwa mkutano mkuu wa kijiji.

Kuwajibishwa

Mwanakamati au mwanakijiji yeyote atakayepatikana na kosa la kutumia vibaya fedha za msitu atawajibishwa na serikali ya kijiji au atashitakiwa katika Baraza la usuluhishi la kata au Mahakama ya mwanzo. Mjumbe yeyote wa Kamati ya Maliasili atakayepatikana na kosa lazima ajiuzulu haraka na nafasi iliyoachwa wazi ijazwe kufuata utaratibu unaokubalika.

Ufuatiliaji

Serikali ya Kijiji itafuatilia shughuli zote zilizopangwa kulingana na mpango kazi wa kila mwaka katika kipindi chote cha miaka mitano. Ufuatiliaji huu utahakikisha kuwa shughuli zote zimefanyika kulingana na mpango kazi.

Kiambatanisho A

Ramani inayoonyesha Mipaka ya Msitu wa Kijiji


RAMANI INAYOONESHA MIPAKA YA MSITU WA HIFADHI WA KIJIJI CHA MTAWATAWA
(12391 Ha)
N
Eneo la Mashamba
Msitu wa kijiji
Legezamwendo
Msitu wa Kitogoro
Msitu wa kijiji
cha Mikunya
Msitu wa kijiji
Nahoro
Kielelezo
Eneo la Asilimia kumi
Mpaka wa Msitu
Eneo la Msitu
0
5000
10000 M
400000.000
405000.000
410000.000
415000.000
420000.000
425000.000
430000.000
8905000.000
8900000.000
8895000.000
8890000.000
8885000.000